**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

**Anwani ya Simu: "ELIMU"**
**DAR ES SALAAM**
**SIMU: 2110146, 211050/2, 2110179**
**Telex: 41742 Elimu Tz**
**Fax: +255-22-2113271**

7 MTAA WA MAGOGONI,
11479 DAR ES SALAAM.

Kumb. Na: ED/OKE/NE/Vol.I/01/43

Tarehe: 7/08/2014

**Katibu Mkuu, OWM-TAMISEMI,**
**Mwenyekiti - TAMONGSCO,**

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2014 KUHUSU UTAYARISHAJI WA VIFAA VYA KUJIFUNZIA NA KUFUNDISHIA**

## 1. UTANGULIZI

Kabla ya mwaka 1991, jukumu la kuandika vitabu lilikuwa la Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ambapo kitabu kimoja cha kiada kilitumika kwa kila somo kwa shule zote Tanzania Bara.

Mwaka 1991 Wizara ilipitisha utaratibu mpya wa Uzalishaji na Usambazaji wa Vitabu Shuleni na Vyuo vya Ualimu. Utaratibu mpya wa pamoja na mambo mengine iliweka mfumo huria wa uzalishaji na usambazaji wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu nchini na ilielekeza Wizara ya Elimu kujitoa katika uandishi wa vitabu na kuacha jukumu hilo kwa wachapishaji binafsi. Aidha utaratibu mpya ilielekeza matumizi ya kitabu cha kiada zaidi ya kimoja kwa kila somo kwa kila darasa.

Ili kutekeleza Waraka wa Elimu Na 2 wa mwaka 1998 ulitolewa ambapo Kitengo cha Usimamizi wa Machapisho na Vifaa vya Kielimu (BMU- Book Management Unit) kilianzishwa. Kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, waraka huo ulifutwa mwaka 2005 kwa Waraka wa Elimu Na. 7 ulioanzisha Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya kielimu nchini (EMAC - Educational Materials Approval Committee).

## 2. HALI HALISI YA UTEKELEZAJI

Pamoja na kutolewa kwa Waraka wa Elimu Na. 7 wa mwaka 2005, bado changamoto za ubora na vitabu na vifaa vingine vya kielimu ziliendelea kujitokeza na hivyo kuathiri ubora wa elimu. Aidha, mwaka 2009, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliagiza matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo na kwa kila darasa nchi nzima. Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza na

kutekeleza agizo hilo ilifanyika tathmini na mchakato wa marekebisho ya mfumo mzima wa uandaaji na utoaji wa ithibati wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu.

Kwa kuzingatia matokeo ya tathmini hiyo na marekebisho ya mfumo huo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mamlaka aliyonayo chini ya "Kifungu Na 5 cha Sheria ya Elimu Sura ya 353" amefuta Sera ya Uzalishaji na Usambazaji wa Vitabu Shuleni na Vyuo vya Ualimu ya Mwaka 1991 na kufuta Waraka wa Elimu Na. 7 wa mwaka 2005 katika mwongozo ulioambatanishwa katika waraka huu. Aidha, utaratibu mpya wa uandaaji na utoaji ithibati wa vitabu na vifaa vingine vya kielimu chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania umeainishwa.

Kufuatia mabadiliko hayo, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) itaandika na kuchapisha vitabu vya kiada (kitabu kimoja kwa kila darasa na kila somo) kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu. Pia itaratibu maandalizi na uzalishaji vitabu vya ziada (reference books) na vifaa vingine vya elimu (vifaa vya kujifunzia na kufundishia) vitakavyoandaliwa na wachapaji binafsi. (Utekelezaji wa jukumu hili umeainishwa katika mwongozo utakaoambatatishwa na Waraka huu).

Waraka huu unafuta Waraka Na. 7 wa mwaka 2005, na unaanza, kutumika kuanzia tarehe 1/9/2014.

Prof. Eustella P. Bhalalusesa
**KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Makatibu Tawala (M)/(W),
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya/Mji/ Manispaa/ Jiji,
Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),
Wakaguzi Wakuu wa Shule Kanda/Wilaya.

**MWONGOZO WA UANDAAJI NA UTOAJI ITHIBATI WA VITABU NA VIFAA VINGINE VYA KIELIMU**

Kufuatia kuvunjwa kwa iliyokuwa Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya Kielimu (EMAC), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhi majukumu ya Uandishi wa vitabu vya Kiada na uratibu wa utoaji wa ithibati kwa vitabu na vifaa vya kielimu kwa Taasisi ya Elimu Tanzania (TET).

Katika kutekeleza majukumu hayo TET itazingatia yafuatayo:

**A. Uandishi wa vitabu na vya kiada ( Text Books)**

1. **Uandishi wenyewe (Writing of Books)**
   Hatua hii itahusisha waandishi wa vitabu (Book writers) na wahariri (Editors).

2. **Uhakiki wa Maudhui (Validation of contents)**
   Majopo ya wataalam wa masomo (subject panels) yatafanya uhakiki wa maudhui. Baada ya uhakiki kukamilika miswada ya vitabu itapelekwa kwenye Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuthibitisha uhakiki uliofanywa na wataalamu wa masomo.

3. **Utoaji wa Ithibati (approval)**
   Miswada ya vitabu vilivyothibitishwa na Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania itapelekwa kwa Kamishna wa Elimu ambaye baada ya kupitia na kujiridhisha nayo kuhusu ubora na viwango, itawasilisha kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndiye atakayeidhinisha (approve) matumizi ya vitabu hivyo.

**B. Uandishi wa vitabu vya ziada (Reference Books)**

1. Hatua hii itahusisha wachapaji binafsi kuwasilisha miswada (Camera Ready copy) TET kwa ajili ya uhakiki.

2. **Uhakiki wa Maudhui (Validation of contents)**
   Majopo ya wataalam wa masomo (subject panels) yatafanya uhakiki wa maudhui. Baada ya uhakiki kukamilika miswada ya vitabu itapelekwa kwenye Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuthibitisha uhakiki uliofanywa na wataalamu wa masomo.

3. **Utoaji wa Ithibati (approval)**
   Vitabu vilivyothibitishwa na Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania vitapelekwa kwa Kamishna wa Elimu ambaye atavipitia na kujiridhisha

na ubora na viwango wa vitabu hivyo, kabla ya kuwasilishwa kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndiye atakayeidhinisha (approve) matumizi ya vitabu hivyo.

**C. Utayarishaji wa vifaa vingine vya Elimu (Other Educational Materials).**
Katika utayarishaji wa vifaa vingine vya elimu hatua zifuatazo zifuatwe:-

1. **Kuandaa kifaa/vifaa**:
   Katika hatua hii waandaaji binafsi watawasilisha Taasisi ya Elimu Tanzania kifaa/vifaa vya kielimu kwa ajili ya uhakiki.

2. **Uhakiki wa kifaa (validation)**
   Wataalam wa masomo (Subject Panels) watafanya uhakiki wa kifaa/vifaa vilivyoandaliwa kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia kama vina maudhui ya somo yanayokusudiwa. Baada ya uhakiki kukamilika kazi husika zitapelekwa kwenye Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuthibitishwa.

3. **Utoaji wa Ithibati (approval)**
   Vifaa vilivyothibitishwa na Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania vitapelekwa kwa Kamishna wa Elimu ambaye atapitia vifaa hivyo ili kujiridhisha kwa ajili ya ithibati (approval) kwa vifaa hivyo kutumika shuleni.

**RUFAA**

i) Iwapo mtu yoyote hataridhika na maamuzi yalitolewa na Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania au na Kamishna wa Elimu anaweza kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya elimu nchini. Aidha uamuzi wa Waziri utakuwa wa mwisho.

ii) Rufaa yoyote inatakiwa kuwasilishwa kwa waziri ndani ya siku 30 baada ya kupokea taarifa ya maandishi kuhusu uamuzi husika.